

**HOTUBA YA MGENI RASMI MHE. KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MB)
WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA
UFUNGUZI WA MKUTANO WA MWAKA WA WADAU WA LISHE,
SEPTEMBER 10, 2019**

Mheshimiwa Jenista Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu,
Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu,

Mheshimiwa Ummy Mwalimu (Mb), Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii,
Jinsia, Wazee na Watoto,

Mheshimiwa Suleiman Jafo (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Mheshimiwa Prof. Joyce Ndalichako (Mb), Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia
na Mafunzo ya Ufundi,

Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Japhet Hasunga (Mb), Waziri wa Kilimo,

Mheshimiwa Luhaga Mpina (Mb), Waziri wa Mifugo na Uvuvi,

Mheshimiwa Innocent Bashungwa (Mb), Waziri wa Viwanda, Biashara na
Uwezesaji,

Mheshimiwa Prof. Makame Mbarawa (Mb), Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Doto Biteko (Mb), Waziri wa Madini,

Waheshimiwa Manaibu Waziri na Makatibu Wakuu,

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Dkt. Bilinith Mahenge; pamoja na
viongozi wengine wa ngazi za Mkoa na Halmashauri mliopo,

Waheshimiwa Wabunge na viongozi wa Vyama vya Siasa,

Waheshimiwa Mabalizi wanaoziwakilisha nchi mbalimbali,

Ndugu Viongozi waandamizi wa Idara, Taasisi, Wakala za Serikali, Wakuu wa
Vyuo vya Elimu ya Juu,

Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa, Wadau wa Maendeleo na Asasi za
Kiraia,

Ndugu Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania,
Ndugu Wageni Waalikwa, Waandishi wa habari na wadau wote wa Lishe,
Mabibi na Mabwana.

Habari za asubuhi

Kwa mara nyingine tena nina furaha kubwa sana kujumuika na wadau wa lishe siku hii ya leo. Hii ni mara yangu ya tatu kuhudhuria mkutano wa mwaka wa wadau wa lishe nchini na hivyo nahisi kuwa mwanafamilia wa wadau waliohamasika katika masuala ya lishe. Awali ya yote napenda kumshukuru Mungu kwa kutuwezesha kukutana tena hapa Jijini Dodoma, kwa ajili ya kupitia, kujadili na kubadilishana uzoefu kuhusu masuala ya lishe.

Mabibi na Mabwana

Niwapongeze Mawaziri, Manaibu Waziri na Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali mlioweza kushiriki katika mkutano huu muhimu. Kuwepo kwenu mahali hapa kunadhihirisha umuhimu wa mchango wa sekta mbalimbali mnazozisimamia katika kuboresha hali ya lishe nchini.

Pia niwashukuru wadau wote wa maendeleo kutoka ndani na nje ya nchi, viongozi wa ngazi mbalimbali za Serikali, viongozi wa asasi za kiraia, viongozi wa madhehebu ya dini na wageni wote mliojitokeza kushiriki katika mkutano huu. Aidha, niwapongeze kamati nzima ya maandalizi chini ya uratibu wa ofisi yangu, kwa mara nyingine kufanikisha maandalizi ya mkutano huu na kuweza kuwaleta wadau wote pamoja.

Mabibi na Mabwana

Mkutano huu wa mwaka ni wa muhimu sana kwani unatuwezesha kujitathmini sisi wenyewe kama watekelezaji wakuu wa masuala ya lishe na kuona ni kwa

kiasi gani tumepiga hatua katika kufikia malengo tuliyojiwekea. Ninafahamu kuwa mwaka jana mliweka maazimio mbalimbali ya kuboresha utekelezaji wa mipango ya lishe. Huu ni wakati wa kutathmini utekelezaji wa maazimio hayo na kuweka mikakati kwa ajili ya kutekeleza yale ambayo tumeshindwa kukamilisha katika kipindi cha mwaka mmoja. Ninafahamu kuwa, tathmini ya baadhi ya mikakati ya kutekeleza Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe zimeanza kufanyika ikiwa ni pamoja na Mkutano wa Tathmini ya Mikataba ya Lishe uliofanyika mwezi Agosti,2019. Tathmini hizo ni muhimu kwani zinajenga msingi imara wa utekelezaji na tathmini ya Mpango wa Taifa wa Lishe. Pamoja na tathmini hizo, Mkutano huu unatoa fursa kwa wadau wote wa lishe kukutana kwa pamoja na kutathmini utekelezaji katika afua zote za lishe tulizojipangia kufanya katika Mpango.

Naomba tutambue kuwa mkutano huu ni muhimu kwa kuwa, kuweka mipango bila kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji ni sawa na kazi bure. Ni lazima mara kwa mara tuwe na uwezo wa kuona yale tuliyoopanga kutekeleza yamefanyika pamoja na kuchukua hatua kutatua changamoto zilizojitokeza. Ni matumaini yangu kuwa wote mtashiriki kikamilifu kikikamilifu kwa kutoa michango na maoni mbalimbali yatakasaidia kuboresha hali ya lishe nchini.

Mabibi na Mabwana

Utupiamlo ni miongoni mwa vikwazo vya kutimiza dhamira ya Serikali ya awamu ya tano ya kujenga uchumi wa viwanda ambao utawezesha Taifa letu kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Bila kuwa na lishe bora na afya njema, vinavyosaidia kuongeza uwezo wa kuelewa na ubunifu ili kuhimili ushindani hatutafika kwa wakati kwenye uchumi wa kati na wa viwanda tunaoutaka. Na ndio maana hata Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka

Mitano 2016/2017- 2020/2021 umeainisha lishe kama moja ya maeneo ya kimkakati katika kufika malengo ya nchi.

Mabibi na Mabwana

Nimefurahi kufahamu kuwa, ajenda kubwa ya mkutano wa mwaka huu ni kupokea na kujadili Matokeo ya Taarifa ya Mapitio ya Kati ya Utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe. Agenda hii ni muhimu sana kwani ni kipimo kitakachotuwezesha kujua iwapo jitihada zetu zinazaa matunda tunayokusudia.

Nikiri kuwa, nimefarijika kuona tumeweza kupiga hatua katika kupunguza kiwango cha udumavu kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano; na kiwango cha upungufu wa damu kwa wanawake walio katika umri wa kuzaa (miaka 15 - 49). Kwenye hili hatuna budi kujipongeza. Hii inaonesha kuwa upo uwezekano wa kufikia malengo tuliyojiwekea kwenye Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe iwapo tutaongeza juhudi.

Mabibi na Mabwana

Pamoja na tafiti kuonesha kwamba tumepunguza viwango vya udumavu na upungufu wa damu bado viwango vyake havikubaliki kimataifa. Vilevile, tuna viwango vya utapiamlo ambavyo vimezidi kuongezeka na havikubaliki kimataifa ikiwemo uzito uliozidi kwa wanawake wenye umri wa kuzaa. Hii ni hatari kubwa kwa nchi yetu inayokabiliwa na aina nyingine za upiamlo unaosababishwa na lishe duni kama vile udumavu, utapiamlo mkali na wa kadiri ambapo athari zake ni kubwa katika ukuaji wa watoto wetu wenye umri wa chini ya miaka mitano. Hali hii ni ishara kwamba tunatakiwa kuongeza juhudi

katika kupambana na aina zote za utapiamlo ili kufikia viwango vinavyokubalika kimataifa.

Ni muhimu kuwa na uwiano katika afua tunazopanga kwa kuangalia aina zote za utapiamlo na makundi yote yaani wanawake, watoto wadogo na wachanga, wazee, vijana na wanaume. Kwa matokeo haya, ipo haja ya kila mdau wa lishe kuchukua hatua za makusudi kuhakikisha tatizo la uzito uliozidi kiasi na vifo vya watoto vinavyochangiwa na utapiamlo mkali na kadiri vinapungua katika jamii yetu. Matokeo ya tafiti hii na nyingine zitupe chachu ya kutafuta suluhisho la kukabiliana na changamoto za utapiamlo huo nchini ili tunapokuja kufanya tathmini ya mwisho tuone mabadiliko chanya katika eneo hili. Ni matumaini yangu kuwa katika hizi siku mbili ambazo mtakuwa mnajadili ripoti hii mtaona namna mtakavyoyatumia matokeo hayo katika kuweka mikakati thabiti na inayotekelezeka na hivyo kusaidia nchi kuboresha hali ya lishe.

Mabibi na Mabwana

Matokeo mazuri ya hali ya lishe yatapatikana kwa kufanya kazi kwa ushirikiano kupitia sekta zetu na miradi tunayoitekeleza. Pamoja na kuwa kuna sababu nyingi za msingi zinazochangia hali duni ya lishe, ni ukweli usiofichika kuwa, ili kupata matokeo bora ya hali ya lishe nchini, ni lazima tuhakikishe tunafanya kazi kwa pamoja kupambana na sababu hizo. Lishe ni suala mtambuka, hivyo hatuna budi kuendelea kushirikiana katika utekelezaji wa mikakati tunayopanga kama taifa ili kuleta matokeo bora kwa wananchi tunaowatumikia.

Mpango Jumuishi wa Lishe wa Miaka Mitano umeainisha majukumu ya kila mdau katika utekelezaji. Ni vizuri kujiuliza, ni kwa kiasi gani sisi sote katika maeneo yetu tumeshiriki katika kutekeleza yale yalioainishwa katika Mpango

huo ili kuchangia uboreshaji wa hali ya lishe nchini. Majibu tutakayopata yatumike kuimarisha michango yetu katika mikakati tuliyonayo hususan maeneo ambayo ripoti imeonyesha hatufanyi vizuri.

Mabibi na Mabwana

Ni vyema kujua eneo la lishe lina fursa nyingi ambazo iwapo kila mmoja wetu atazitumia kikamilifu Taifa letu litanufaika. Sehemu kubwa ya manufaa hayo ni pamoja na sekta za uzalishaji pamoja na uwezo wa kuongeza virutubisho kwa kutumia viwanda ndani ya nchi. Ni matumaini yangu kuwa, fursa hii ya mkutano itatumiwa kujifunza, kujenga uelewa wa pamoja na kuonesha mikakati na mbinu mbalimbali zinazoweza kutumika nchini kuboresha hali ya lishe kwa Watanzania. Baada ya kujitosheleza, fursa kwa majirani zetu zitumike kikamilifu kuimarisha hali ya lishe katika kanda na Afrika kwa ujumla.

Mabibi na Mabwana

Tafiti ni moja ya maeneo muhimu tunayoweza kutumia kutatua matatizo ya lishe kwenye mazingira yetu. Nizikumbushe Taasisi zinazojihusisha na tafiti ikiwa ni pamoja na Taasisi za Serikali na zile za binafsi kuibua zinazosaidia kutoa majibu na mapendekezo ya kutatua matatizo ya lishe yanayoikabili jamii yetu. Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania iendeleo kuweka mazingira mazuri ya kuhamasisha uendeshaji wa tafiti za lishe na kulishauri Taifa juu ya lishe bora kama ilivyoainishwa katika Sheria iliyoanzisha Taasisi hiyo ya mwaka 1973 .

Aidha, tukumbuke kuwa mipango yoyote tunayojiwekea haiwezi kuleta matokeo chanya bila kuitengenezea mikakati thabiti ya utekelezaji ikiwa ni pamoja na kutenga rasilimali za kutosha. Ni matumaini yangu kuwa kundi hili kubwa la wataalam kutoka sekta mbalimbali litajadili mbinu na kuibua mikakati

itakayoweza kutumika katika kupunguza tatizo la utapiamlo ikiwa ni pamoja na kuainisha rasilimali zinazohitajika, mbinu za kuongeza mchango wa wadau na kutumia rasilimali tulizonazo kwa ufanisi.

Mabibi na Mabwana

Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua kuwa utekelezaji wa shughuli za lishe unahitaji mazingira wezeshi ili kufanikiwa. Kwa kutambua umuhimu huo, napenda niwahakikishie kwamba, Serikali itaendelea kuweka mikakati ya kisera itakayoweza kukabiliana na aina zote za utapiamlo ili kuhakikisha kuwa Taifa letu linakuwa miongoni mwa nchi zinazofanya vizuri katika eneo la lishe katika bara la Afrika na dunia kwa ujumla. Hii itawezekana kwa kudumisha utawala bora kwenye masuala ya lishe, kuongeza ushiriki na uwajibikaji wa sekta mtambuka pamoja na kuhakikisha tunafuatilia kwa kina utekelezaji wa mipango na ukusanyaji wa rasilimali kwa ajili ya lishe.

Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau itaendelea kutoa kipaumbele kwa maeneo ambayo yameathirika zaidi na ambayo yanatekeleza miradi inayolenga kupunguza udumavu kwa watoto; matatizo ya upungufu wa vitamin na madini; kuimarisha matibabu ya utapiamlo mkali na wa kadiri; kupunguza tatizo la uzito uliokithiri na viriba tumbo na tatizo la upungufu wa damu kwa wanawake na watoto ili kuhakikisha kuwa miradi hiyo inaleta matokeo chanya katika maeneo hayo.

Mabibi na Mabwana

Rai yangu kwenu nyote, ni kuhakikisha kuwa kila mmoja kwa nafasi yake anaunga mkono jitahada za Serikali katika kutokomeza utapiamlo. Natoa wito kwa Watendaji Wakuu wote katika wizara, idara, wakala na taasisi za Serikali lakini pia wadau wa maendeleo, asasi za kijamii kuhakikisha mnaweka malengo ya lishe katika mipango yenu ya kila mwaka; na kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe.

Napenda kuchukua fursa hii kuwasihi sana wadau wote wa Lishe mlioshiriki na wale ambao hawajashiriki kwenye Mkutano huu kutumia mapendekezo yalioainishwa katika Ripoti hii kupanga mipanfo yenu kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2020/21 kwa kutoa kipaumbele katika maeneo ambayo bado hatufanyi vizuri. Aidha, viongozi wa ngazi za Mikoa na Halmashauri zote nchini wahakikishe afua zilizoainishwa katika Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe zinajumuishwa katika mipango na bajeti za kila mwaka sambamba na kutoa fedha zilizopangwa kwa ajili ya utekelezaji.

Mabibi na Mabwana

Kabla ya kuhitimisha hotuba yangu nitumie fursa hii kuwashukuru wadau wa maendeleo nchini kwa kutuunga mkono katika kuwezesha uendeshaji wa mkutano huu. Serikali inathamini michango yenu na kuomba kuendelea kupanua wigo katika masuala mbalimbali ya lishe ili kutimiza malengo tuliojiwekea. Mwisho nizidi kuisitiza kuwa maazimio mtakayokubaliana katika mkutano huu yazingatiwe na kila mmoja wetu ili kuupa tija mkutano huu.

Kwa maneno hayo sasa napenda kutamka rasmi kuwa; Mkutano wa Sita wa Wadau Kutathmini Utekelezaji wa Masuala ya Lishe nchini umefunguliwa. Nawatakieni nyote mkutano wenye tija.

Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Afrika.

Ahsanteni kwa kunisikiliza